

**SALAMU ZA MKUU WA MKOA WA PWANI MHESHIMIWA  
ENG. EVARIST NDIKILO KATIKA KIKAO KAZI NA  
WAHESHIMIWA WAKUU WA WILAYA KUJADILI  
MIGOGORO YA ARDHI, KERO ZA WANANCHI NA  
KUWEKA MPANGO WA KUZITATUA  
TAREHE 11 AGOSTI 2020**

- *Ndugu Katibu Tawala wa Mkoa,*
- *Wahe. Wakuu wa Wilaya,*
- *Wajumbe wa Kamati ya Usalama Mkoa,*
- *Wakuu wa Taasisi mbalimbali za Serikali Ngazi ya Mkoa,*
- *Wakurugenzi na Mkurugenzi wa Halmashauri,*
- *Wataalamu ngazi ya Mkoa na Halmashauri.*

**Ndugu Washiriki,**

Awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kutuwezesha kukutana hapa leo.

Nimeitisha Kikao Kazi hiki mahususi kwa ajili ya kujadili Migogoro ya Ardhi, Miradi ya Serikali inayotekelezwa na kupokea mawasilisho ya kero mbalimbali za Wananchi kutoka kwenye Maeneo yenu.

Nafahamu nilitoa maelekezo ya kutenga siku katika juma ya kusikiliza na kupokea kero za Wananchi, taarifa mlizowasilisha tunazo za siku za kusikiliza kero. Aidha, niwaombe msiishie hapo

bali muwafuate Wananchi walipo na kutatua kero zao kwenye maeneo yao.

Ni matumaini yangu ratiba hizi zikifuatwa kikamilifu kutapunguza malalamiko ya Wananchi kwa kero zilizo ndani ya uwezo wetu wa Wilaya na Mkoa. Pia kutapunguza wananchi kukimbilia kwa Viongozi wa Juu kulalamikia kero ambazo zipo ndani ya uwezo wetu.

Nimuagize pia Katibu Tawala Mkoa aimarishe Ofisi ya Malalamiko hapa Ofisi ya Mkuu wa Mkoa. Ateuliwe Afisa ambaye atafanya kazi hii kwa weledi na umahiri mkubwa. Aidha, asaidiwe na kamati ndogo ambayo itahusisha Mwanasheria, Katibu Tawala Miundombinu, Afisa Utumishi, Afisa Ustawi wa Jamii na wengine wachache utakaona inafaa.

### ***Ndugu Washiriki,***

Kwa kipindi kirefu Mhe. Rais amekuwa akituasa sisi wasaidizi wake kuwa hatumuelewi, amekuwa akifikia hatua ya kutengua teuzi na kuweka watu wengine ili kuleta tija katika utendaji. Tumeona tarehe 30 Julai 2020 Mhe. Rais alipokuwa akisalimia Wananchi katika Wilaya za **Rufiji, Kibiti na Mkuranga** Wananchi walipokuwa wakiwasilisha Malalamiko yao kana kwamba hakuna Viongozi wanaomsaidia Mhe. Rais katika Wilaya hizo na Mkoa. Ilijitokeza pia tarehe 7 Agosti 2020 wakati wa Ziara ya Mhe. Waziri Mkuu alipotembelea Mradi wa Ujenzi wa Reli ya Mwendokasi (SGR) Ruvu Wilaya ya Kibaha, Wananchi walikuwa na Malalamiko na Kero nyingi hadi kufikia hatua Mhe. Waziri Mkuu kuniagiza kwenda kusikiliza kero za Wananchi hao na kuzitafutia ufumbuzi siku inayofuata tarehe 8 Agosti 2020.

Mambo haya yanapotokea kwenye Mkoa ni ishara kuwa hatupo vizuri katika kushughulikia kero za Wananchi, hata hivyo tumejaliwa kuwa kwenye Mkoa ambao Wananchi wake wanajua

kujieleza vizuri hivyo kuzungumza kwao sio tatizo **ni lazima tujipange vizuri Viongozi wenzangu kuzitafutia ufumbuzi changamoto zao.**

***Ndugu Washiriki,***

***Jambo ambalo limekuwa sugu katika Mkoa wetu ni Migogoro ya Ardhi kama ifuatavyo:-***

- i. Migogoro wa Ardhi kati ya Wakulima na Wafugaji,
- ii. Migogoro ya Mipaka kati ya Maeneo ya Jeshi (TPDF, Magereza, JKT na Vijiji),
- iii. Migogoro ya Ardhi kati ya Wawekezaji/Makampuni binafsi na Wanachi,
- iv. Wawekezaji kuhodhi ardhi kubwa muda mrefu bila kuiendeleza,
- v. Migogoro wa Mipaka kati ya Kijiji kimoja na Kingine kati Wilaya na Wilaya au kati ya Mkoa na Mkoa,
- vi. Wananchi kuvamia ardhi yenye hati miliki na kuiendeleza kwa ajili ya makazi na shughuli za kilimo,
- vii. Migogoro ya Ardhi kati ya Taasisi binafsi, Taasisi za Serikali na Wananchi,
- viii. Nakadhalika.

Aidha, kuna kero zingine za Wananchi za kukosa Miuondombinu Muhimu ya Kijamii, kama vile:-

Umeme, Shule, Zahanati au Kituo cha Afya, Kituo cha Polisi, Magari ya Kubebea wagonjwa, Madawati mashuleni, Vyoo kwenye shule stendi na Sokoni.

Malalamiko mengine ni kucheleweshewa Haki kutoka vyombo vya Sheria, kushindwa kutekeleza Hukumu mara baada ya hukumu kutolewa, Wafanyakazi kufukuzwa kazi na Makampuni ya Viwanda bila kufuata taratibu za sheria na kutolipwa stahiki zao.

***Ndugu Washiriki,***

Siku ya leo nimeona niwaite hapa kwa lengo la kubadilishana uzoefu na kujadiliana mipango mizuri ya kutatua changamoto zote tulizonazo. Niwaombe tuwe makini katika mawasilisho yote na kuchangia ipasavyo.

Baada ya kusema hayo, **natamka rasmi Kikao Kazi cha siku moja cha kujadili Migogoro ya Ardhi, Miradi ya Serikali inayotekelezwa na kupokea kero mbalimbali za Wananchi kimefunguliwa rasmi.**

**ASANTENI KWA KUNISIKILIZA**